**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION**

**121/1** **KISWAHILI 1**

(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3** **Alhamisi, 04 Mei 2017 mchana**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina maswali **kumi (10)** katika sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **saba (7)** kwa kuzingatia maelekezo kutoka katika kila sehemu.
3. Kila sehemu ina alama **ishirini (20)**.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Vikokotozi **haviruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 20)**
**UFAHAMU**
Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kwa umakini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu kwa usahihi maswali yanayofuata.

Vitabu ni rafiki kwa wanadamu. Viko chini ya amri siku zote. Ukurasa wa kitabu kilichopigwa chapa ni usemi bora usiotoweka maishani. Huwapa mafundisho na faida kubwa watu wazingatiapo. Vitabu ni **hazina** bora kuliko hazina ya mfalme yeyote katika dunia hii. Ni machimbo azizi ya usanifu, maandiko, ujuzi na maarifa. Kitabu kizuri ni rafiki, mwalimu na kiongozi wa watu katika maisha.

Iliwapasa babu zetu kwenda safari kubwa kusikiliza maneno ya mtu mwenye hekima. Sasa hekima imo katika vitabu mezani petu inatungoja. Kwa kweli, kuna vitabu vingi sana. Husemwa kwamba kuna vitabu vya **kitambo**, tusomavyo kisha tukavitupa. Kuna vitabu vya nyakati zote, tupendavyo kusoma mara kwa mara, kama mpenzi asomavyo mara kwa mara barua ya kipenzi chake. Hivyo, katika wakati huu uliojaa vitabu vizuri ni vibaya, uchaguzi wa vitabu ni mashaka makubwa. Tusiharibu wakati wetu ujao kwa kitabu chochote hafifu, ambacho sifa yake kubwa ni jina zuri na jalada la kupendeza tu, "nyumba nzuri si mlango, fungua uingie ndani."

Imesemwa kwamba vitabu fulani vinapaswa kujaribiwa, yaani tupekue kurasa zake na tutazame yaliyomo, baadhi yake lazima yamezwe, yaani visomwe vyote toka jalada hata jalada na vingine vichache vimebidi kutafunwa na kuyeyushwa, yaani visomwe mara kwa mara. Ni bora kusoma kwa kujifundisha kuliko kwa kujiburudisha, ingawa kusoma kwa kujiburudisha kuna manufaa yake, hasa kwa mtu mwenye kazi ngumu. Kuna vitabu bora vya zamani na vya sasa vya kusoma vilevile. Swali tunalojiuliza visomwe vipi? Rai iliyotolewa ni kwamba ili kupata ujuzi, lazima tusome vitabu vipya kabisa, pia twaweza kusoma vitabu vya zamani kabisa ila kwa jicho la uhakiki. Ila kuna usemi usemao "ukitaka kumficha mjinga mpe kitabu."

Vitabu vibaya vikiingia mikononi mwa vijana, akili zao huambukizwa na maongozi yake maovu. Vijana wengi hodari wameangamia, kwa sababu ya kusoma vitabu vibaya. Vitabu vizuri **hutakasa**, hukuza tena hustawisha akili, hujenga na tabia yetu. Vitabu vya historia hutia busara, mashairi huleta akili na hesabu huongeza werevu. Lakini kila mtu kila mtu akubali kwamba kusoma kunamsitawisha mtu.

Faida nyingine ya kusoma vitabu ni kwa mtu hasa aliyeacha masomo yake ya desturi, kwake vitabu ni aendeleo ya elimu. Aweza kufululiza masomo yake nyumbani. Kitabu kizuri ni rafiki bora kabisa atakuongoza **peponi**.

**Maswali**

(a) Andika kichwa cha habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi matano.

(b) Eleza mawazo makuu mawili ya mwandishi.


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

(c) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika habari hii.
   (i) Hazina
   (ii) Kitambo
   (iii) Hutakasa
   (iv) Peponi

(d) Mwandishi anaposema "nyumba nzuri si mlango, fungua uingie ndani" anamaanisha nini?"

(e) Nini maana ya usemi "ukitaka kumficha mjinga mpe kitabu."

(f) Ili tuweze kupata maarifa, mwandishi anashauri tusome vitabu gani?

2. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno **mia moja na ishirini**.

**SEHEMU B (Alama 20)**

**MATUMIZI YA SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

3. (a) Eleza maana ya viambishi vya **O-rejeshi**.

   (b) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia **O-rejeshi**.
   (i) Kanu ameleta mpira wa miguu. Ulikuwa unahitajika mpira.
   (ii) Rukia anatafuta vitabu. Vitabu vimekwisha.
   (iii) Gazeti lilichapwa. Gazeti limekwisha.
   (iv) Mtoto ametekwa nyara. Mtoto ameptaikana.
   (v) Yule msichana amesimama pale. Yule msichana ni dada yangu.

4. Kwa kutumia mifano bainisha kazi mbili za mnyumbuliko na kazi tatu za uambishaji katika lugha ya Kiswahili.

5. Mtumiaji wa lugha ya Kiswahili ambaye ni mahiri wa lugha zingine, umahiri wake hukabiliwa na changamoto mbalimbali. Kwa kutumia hoja nne na mifano, fafanua changamoto hizo.

6. Bainisha matumizi ya "ki" iliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:
   (i) Kiti <u>ki</u>dogo
   (ii) A<u>ki</u>ja apewe mzigo wake
   (iii) Kitabu <u>ki</u>mechanika
   (iv) Kiti <u>ki</u> kidogo
   (v) Wana<u>ki</u>subiria
   (vi) Analima a<u>ki</u>imba
   (vii) Atavuna alicho<u>ki</u>panda


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

(viii) Kitoto hiki sikiwezi
(ix) Aliruka juu kihuni
(x) Anacheza kitoto

**SEHEMU C (Alama 20)**
**UTUNGAJI**
Jibu swali la **saba (7)**.

7. (a) Taja na kueleza mambo muhimu saba ya kuzingatia katika kuandika kadi ya mwaliko.

(b) Jifanye wewe ni mzazi wa mwanafunzi **Sikujua Kizito** anayehitimu Kidato cha Sita mwaka 2017. Andika kadi ya mwaliko kuwaalika ndugu, jamaa na marafiki katika sherehe ya kumpongeza mtoto wako itakayofanyika tarehe 7/6/2017. Jina lako liwe **Sikutegemea Kizito**.

**SEHEMU D (Alama 20)**
**MAENDELEO YA KISWAHILI**
Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

8. Waingereza na Waarabu walidumaza maendeleo ya Kiswahili wakati wa ukoloni nchini Tanzania. Thibitisha dai hilo kwa kutumia hoja nne kwa Waingereza na hoja nne kwa Waarabu.

9. Eleza kazi za BAKITA na UKUTA katika kukuza na kueneza Kiswahili. Toa hoja tatu za BAKITA na hoja tatu za UKUTA.

**SEHEMU E (Alama 20)**
**TAFSIRI**
Jibu swali la **kumi (10)**.

10. "Kazi ya kutafsiri ina taratibu mahususi." Fafanua dai hili kwa kueleza mambo muhimu sita ya kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri.


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org